# Umeme urithi muhimu katika maendeleo

Na Beda Msimbe

WAKATI Serikali inapendekeza bajeti yake ya mwaka huu, moja ya mambo ambayo yaliombwa na wenye viwanda yazingatiwe kwa makini ni upatikanaji wa umeme wenye uhakika.

Kauli ya Shirikisho la Wenye Viwanda (CIT) inasema umeme wenye uhakika na bei nafuu ndio utakaoipandisha nchi katika sekta ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani na kusukuma mbele uchumi.

Kwa namna yoyote ile umeme ndio nguzo kubwa ya uzalishaji kuanzia uchakataji, usindikaji hadi bidhaa iliyokamilika.

Katika mapendekezo yao siyo tu walisema haja ya nchi kuwa na umeme wa uhakika lakini pia haja ya kuoanisha utendaji wa sekta mbalimbali zinazowezesha kukua kwa viwanda na uwekezaji.

Mpaka mwaka 2011 umeme umekuwa changamoto kubwa katika uchumi wa Tanzania, ukisukuma nyuma mafanikio machache yaliyokuwapo kabla ya mwaka 2010.

Tatizo la kupatikana kwa umeme, au tuseme umeme usiokuwa na uhakika umeharibu mambo mengi ambayo ndio msingi hasa wa uzalishaji.

Kukosekana kwa umeme wa uhakika kati ya mwaka 2010 hadi 2012 imekuwa tatizo kubwa kwa taifa hasa pale ambapo wazalishaji 60 wakubwa na wa kati walipojikuta wakipunguza uzalishaji na wale wanaoendesha sekta ya huduma wakiongeza gharama kufidia utumiaji wa majenereta.

Katika kuangalia ukuaji wa uchumi , inaaminika kwamba ifikapo mwaka 2020 mahitaji ya umeme nchini yatakuwa juu kwa asilimia 42 kutoka mahitaji ya sasa ya asilimia 14.

Lakini pamoja na hilo kujulikana, ni dhahiri kwamba upatikanaji wa umeme kwa sasa ni wa shida kubwa, usioaminika na aghali, hivyo kuchafua kabisa malengo ya wawekezaji.

Katika mazungumzo kwa njia ya simu na Mtendaji wa Shirikisho la Wasindika Maziwa (TAMPA), Edimund Marriki anasema sekta ya maziwa nchini inashindwa kukua kutokana na kutokuwapo kwa umeme wa uhakika kwa vile unakatika katika na ni ghali.

Marriki anasema ingawa kwa sasa umeme unaanza kuonekana kuwa wa kuaminika, bei yake ni tatizo kubwa. Lakini tatizo kubwa kwa wazalisha maziwa analoliona ni kukosekana kwa umeme vijijini ambako anasema kunachangia kwa kiasi kikuwa kudidimiza sekta ya maziwa nchini.

"Huwezi kukuza sekta hii bila kuwa na umeme tena wa uhakika hadi vijijini. Unahitaji vituo vya kukusanyia maziwa na vituo hivi lazima viwe na matangi ya kupoozea maziwa ili yasiharibike," anasema Marriki na kuongeza kwamba vituo hivyo haviwezi kuendeshwa na majenereta kwa sababu ni gharama kubwa.

Anasisitiza kwamba umeme ni msingi mkubwa wa maendeleo ya sekta ya maziwa, kwani hata kama wafugaji watakuwa na mamia ya ng'ombe wa maziwa wasipokuwa na kituo cha kukusanyia maziwa ni kazi bure.

"Ukweli ni kuwa hakuna mwekezaji anaweza kuanzisha kituo cha kukusanyia maziwa kama hakuna uhakika wa umeme kwa ajili ya matangi yake ya kupoozea maziwa ili yasiharibike. Huwezi kuendesha kituo hicho na umeme wa jenereta. Ndio maana wakulima wenye kujiweza huyahifadhi kwa mitambo ya bayogesi na hii ni kwa kiasi kidogo tu," anasema Marriki na kuomba Serikali ikazane kuhakikisha umeme wa uhakika unapatikana hadi vijijini kama itataka watu wapate maendeleo na kuwavutia wawekezaji.

Anasema kwa sekta ya maziwa toka yanatoka katika kiwele cha ng'ombe kazi yake ni kuhifadhiwa au la hayatafika kiwandani.

Anasema mkakati wa kupeleka umeme vijijini na kuusambaza vya kutosha ni muhimu uambatane na kushusha bei yake ili wawekezaji waweze kumudu, hasa wazawa.

Akizungumza na jumuiya ya wafanyabiashara jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, Rais Barack Obama wa Marekani alisema namna nzuri ya kuunga shughuli za uchumi za vijijini na mijini ni kusambaza umeme vijijini. Kadhalika Rais Obama anaamini ukiwawezesha wakulima vijijini, basi unatengeneza pia soko la kununua biadhaa za viwandani.

Pamoja na juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwapo kwa umeme kuonekana kuzaa matunda hasa baada ya kuanza kwa matumizi ya gesi kuzalisha umeme, bado inaonekana kwamba hitilafu za umeme zipo na zinakera.

Watu wenye mahoteli wamesema kwamba tatizo lao kubwa ni ughali wa umeme sambamba na kupatikana kwake.

"Kwani mara nyingi kutokana kukatikakatika kwa umeme tunalazimika kutumia majenereta na hivyo kuongeza gharama," anasema Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Hoteli (HAT), Damas Mfugale, katika mahojiano.

Mzee Mfugale anayemiliki Hoteli ya kitalii ya Peacock ya jijini Dar es Salaam anasema pamoja na kutakiwa kulipa malipo mengine ya kila mwezi, umeme unapokatika husababisha matumizi ya dizeli katika kuhakikisha huduma zinaendelea na hivyo kuondoa hata ile faida kidogo ambayo wenye mahoteli wanapata.

"Kitendo cha mwaka mzima kuwa na tatizo la umeme, kunafanya uwekezaji kuwa mgumu," anasema Mfugale ambaye pia alisema hata wazo lao kwa Serikali la kupunguza bei ya dizeli ili waweze kumudu gharama halikusikilizwa.

Tanzania ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikitegemea sana umeme unaotokana na maji imejikuta katika mazingira magumu kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha kupungua kwa mvua na hivyo mabwawa kukosa maji ya kutosha ya kufua umeme.

Pamoja na tatizo la umeme, bei ya umeme imelalamikiwa sana na Mfugale ambaye anasema inafanya kila kitu katika utoaji wa huduma kuwa ghali.

Si wenye hoteli tu wanasema umeme ni ghali lakini ongezeko la bei katika mwaka huu lilipingwa na Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI) walipinga ongezeko la kodi la asilimia 25 katika umeme na kusema itafanya bidhaa za Tanzania kutokuwa na ushindani.

Mwenyekiti wa CTI, Felix Mosha alishawahi kukaririwa akisema kwamba ongezeko hilo si la kawaida na halifai, badala yake akaitaka serikali iongeze upatikanaji wa umeme na kupunguza bei ili kuchochea uwekezaji.

Mosha katika mazungumzo na waandishi wa habari alitaka mabadiliko ili kuongeza upatikanaji wa umeme kwa kupunguza upotevu wake na kutaka menejimenti ya umeme ijipange katika kuhakikisha inapunguza kupotea kwa umeme na ughali wa umeme.

Mosha alisema umeme wa Tanzania ni aghali zaidi kuliko majirani na kwamba baada ya kupandishwa kwa umeme kufikia asilimia 40.29 Watanzania watalipa senti za Marekani 11 kwa kWh, wakati mataifa mengine kama Afrika Kusini na Zambia ni kidogo.

Utafiti uliofanywa kwa msaada wa BEST AC, CTI zimebainisha mambo mengi kuhusu umeme na kuitaka Serikali kuangalia mambo hayo kama inataka sekta ya viwanda kujiimarisha na kunyanyua uchumi.

Kwa mujibu wa utafiti wa CTI ambao umechapishwa katika majalada kadhaa, pamoja na juhudi zote za Serikali za kuondoa matatizo ya umeme kuna matatizo makubwa yanayozuia maendeleo ya kisekta.

Imebainishwa katika utafiti huo kwamba kukatika kwa umeme kunaleta hasara ya Sh bilioni 31 kwa mwaka pamoja na majenereta kutumika na kwamba Serikali inapoteza kodi ya zaidi ya dola bilioni 9.5 kwa mwaka kutokana na tatizo la umeme.

Mfugale anasema umeme unachangia sana kudumaza huduma zao na kwamba katika mazingira ya bei juu ya umeme na upatikanaji usiokuwa wa kawaida unafanya hali isiwe njema na wawekezaji kuogopa kuwekeza zaidi.

Mwananchi mmoja, Abasi Sultani wa Tandika amesema kwamba kama wananchi wananunua umeme aghali hawezi kufikiri kwamba viwanda vinaweza kutengeneza bidhaa zenye ushindani.

Anasema kwa maoni yake umeme ni ghali hata kwa wasiokuwa na viwanda na unachangia kudumaza msingi wa maendeleo wa kuwapo na nishati ya uhakika na ya bei nafuu.


Anasema ughali wa umeme unachangia pia uharibifu wa mazingira kwa sababu majiko ya kutumia umeme yanakimbiwa na hivyo wananchi wengi kutumia mkaa ama kuni hata kama wana umeme majumbani mwao.

"Kwa kweli gharama za sasa kwa mwezi ni balaa kwa mtu wa kipato cha kawaida," anasema.

Pamoja na maelezo yote bado yapo matumaini makubwa ya mambo kubadilika, pengine mazungumzo yanayofanywa sasa na wawekezaji wakubwa nchini kuona hali ya mazingira ya uwekezaji kwa utafiti uliofanywa na BEST AC kwa mwaka uliopita unaweza kutoa mwanga kuhusu nini kinafaa kufanyika kurekebisha tatizo la umeme kwanza upatikanaji wake na pia bei yake.

Ujio wa Rais wa Marekani nchini ambaye ametangaza nchi yake kuwekeza katika umeme ni faraja nyingine na hasa kama umeme huo utapatikana kwa wingi na kwa bei rahisi. Lakini kubwa ambalo Watanzania wanalitegemea ni ugunduzi wa gesi nyingi nchini mwetu ambao unatarajia kuimarisha upatikanaji wa umeme.

Hata hivyo, wapo wanaopata hofu na ugunduzi huo wa gesi kwamba unaweza usiwe na manufaa makubwa kwani wakati wa ujio wa gesi ya Songosongo iliaminika kwamba gharama za umeme zingepungua lakini hali haikuwa hivyo.



**Unaweza kufuga ng'ombe wengi kama hawa lakini kama hakuna umeme vijijini wa kuwezesha kuhifadhi maziwa kwa barafu hayawezi kufika kiwandani na hivyo wafugaji wataendelea kuwa maskini.**



**Waziri wa Nishati na Madini, Profesa Sospeter Muhongo. Moja ya kazi kubwa ya wizara yake ni kuhakikisha umeme wa uhakika na wenye gharama nafuu unapatikana.**